Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. Dkt. Yahya Nawanda akionesha mpaka wa shamba lake la kunenepeshea ng'ombe lililopo eneo la Lamadi mkoani humo.

RC Simiyu atajwa kubadili fikra za wafugaji Simiyu

Na STANLEY BRYTON

UFUGAJI usiofuata mbinu bora za ufugaji imekuwa ni jambo la kawaida kwa wafugaji wengi nchini na kusababisha kushindwa kupata faida kubwa katika ufugaji wanaoufanya.

Jambo hilo limekuwa ni desturi ya kila mtanzania kufuga ng'ombe pasipo kuzingatia mbinu bora za ufugaji. Kutozingatia njia sahihi za ufugaji bora na kisasa kunawafanya wafugaji kutopata faida kubwa.

Pia, kunasababishwa m mifugo kukosa afya bora, mifugo ikikosa afya bora inakuwa na haina tija kwa wafugaji kwa kuwa mifugo iliyonenepa vizuri inasaidia kukuza kipato cha mfugaji na taifa zima kwa ujumla.

Baadhi ya wafugaji wengi hapa nchini, wanashindwa kuelewa tofauti kati ya ufugaji na uchungaji ng'ombe. Watanzania wengi wamekuwa wakifanya shughuli za kuchunga ng'ombe na sio kuwafuga.

Wafugaji wengine hawana elimu ya kutosha juu ya faida na njia bora za unenepeshaji wa ng'ombe.

Ufugaji wa ng'ombe kwa njia ya kunenepesha ni kitendo cha kuwaweka na kutunza wanyama katika zizi bora na kuwapa chakula kwa kuzingatia lishe bora na kanuni za ugawaji wa lishe na mpangilio wa chakula, utunzaji wa wanyama kwa kuzingatia kanuni bora za utunzaji, matumizi sahihi ya dawa pindi wanapopata athari za magonjwa.

Hii ni miongoni mwa shughuli yenye faida kubwa kwa mfugaji ambayo huweza kumuingizia kipato chake binafsi na kusaidia kuchangia kwenye pato la Taifa kwa ujumla.

Katika kilele cha siku ya maadhimisho ya Nanenane yaliyofanyika mwaka huu jijini Mbeya, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alisema ufugaji wa viumbe majini na mifugo mingine ndio utakayonyanyua ajira kwa wanawake na vijana hapa nchini.

Pia Agosti 12, 2022, Rais Dk. Samia alipokuwa akizungumza na wananchi wa Iringa katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika viwanja vya Samora mkoani humo, aliagiza wananchi wapewe elimu juu ya ufugaji kwa kuzingatia mahitaji ya soko na kupata manufaa makubwa.

Kupitia maagizo hayo ya Rais, Dk. Samia, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia kwa Waziri Abdallah Ulega, imefanyia kazi maagizo hayo ya Rais kwa kuhakikisha programu ya "Jenga Kesho iliyo Bora" (BBT Life) inawainua vijana wote wa Kitanzania.

Na moja ya mikoa inayoitendea haki programu hiyo ingawa bado awamu ya utekelezaji haijafika ni mkoa wa Simiyu.

Mkoa huo unaitendea haki programu hiyo kupitia mfano wa vitendo unaooneshwa na Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Yahya Nawanda ambaye kiasili ni mkulima wa Korosho na Ufuta kutoka mkoani Mtwara.

Mara baada ya kuelimishwa na Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji nchini, Murida Mshota, Dk. Nawanda amehamishia shughuli zake za ujasiriamali katika ufugaji ambapo ametenga eneo kubwa la kufanyia shughuli za unenepeshaji eneo la Lamadi.

Katika eneo hilo hadi sasa amefikisha jumla ya ng'ombe 70 ikiwa ni awamu ya pili ya ng'ombe wa awali ambao aliwauza shilingi milioni 31.

Ni juhudi hizo ndio zilimfanya Mkurugenzi wa Utafiti, Mafunzo na Ugani kwa upande wa sekta ya Mifugo, Dk. Angello Mwilawa, kumtembelea Dk. Nawanda kuona namna anavyotekeleza shughuli zake na kumshauri namna bora ya kufanya shughuli hiyo.

Lililomvutia zaidi Dk. Mwilawa ni juhudi za makusudi zinazofanywa na Dk. Nawanda katika kuhakikisha unenepeshaji wa mifugo unakuwa ni mwarobaini wa migogoro ya watumiaji wa ardhi huku pia ukibadili mifumo ya wafugaji wa mkoa huo kutoka kufuga kiholela mpaka kufuga kisasa.

"Binafsi niliposikia Wizara inatekeleza programu hii nilivutika kuifahamu kwa kina na baada ya kuona ina manufaa nikasema ngoja nianze kuifanya kabla sijahamasisha wananchi wangu kwa sababu sote tunajua kuona ni kuamini" alisema Dk. Nawanda.

Ukifika katika zizi ng'ombe wanaonenepeshwa na Dk. Nawanda utastaajabu uzuri na afya bora ya mifugo yake ingawa yeye anasema utaalam anaotumia ni wa chini sana ukilinganisha na ule unaotumiwa na vijana waliopo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Uzoefu juu ya Ufugaji na Unenepeshaji Ng'ombe

Kwa kawaida imezoeleka kuwa kila jamii ina shughuli zao na taratibu zao tofauti na jamii nyingine katika kujipatia kipato. Na wengi wanaamini kuwa yeye akitoka kabila fulani basi shughuli yao ni fulani.

Imezoeleka wamasai na wasukuma ndio jamii za wafugaji. Lakini kwa vijana wa Simiyu imekuwa tofauti, sio wasukuma wote ndio wanaofanya hii shughuli za unenepeshaji ng'ombe mkoani humo.

Na hii yote imetokana na ushawishi wa Nawanda kwa kwa vijana hao. Dk. Nawanda anaamini kufuga ni kujifunza hasa kutokana na ukweli kuwa hakuwahi kufanya shughuli hiyo kabla.

Baba yake alikuwa anafuga mbuzi na hajawahi kufuga ng'ombe maishani mwake. Na katika familia yao hakuna aliewahi kufuga ng'ombe.

Sababu za kuanza shughuli za ufugaji

Vijana wengi wamezoea kazi za kupata pesa kwa haraka pasipo kuwa wavumilivu, na wamekuwa wavivu wa kujifunza kutoka kwa waliofanikiwa. Wao huona maisha ni rahisi na wakiona mtu kafanikiwa wanaona ni jambo la kawaida tu bila kujua mtu alipotoka.

Wasilolijua wengi ni kuwa Dk. Nawanda alipokuwa mkuu wa Wilaya ya Iramba alikutana na mama mmoja anaitwa Grace Meshack, ambaye ndo alikuwa anamuachia kiti hicho kwa wakati huo.

Wakati mama Grace Meshack anahama alikusudia kumuachia kuku wawili lakini aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Mkalama wakati huo, Moshi Chang'a, akamwambia mama Grace asimpe Dk. Nawanda kuku hao kuku bure, bali atamnunulia kwa shilingi elfu 20.

Baada ya miezi kadhaa kuku hao waliongezeka maradufu na akahamasisha wananchi wa Iramba na Urambo aliohudumu kama Mkuu wa Wilaya kufuga kuku kwa wingi kiasi cha kubadili jina la Dk. Nawanda hadi kuitwa "DC wa kuku".

Pia, fedha iliyotokana na kuuza kuku hao ndio aliyotumia kununua ng'ombe aliowanenepesha mkoani Simiyu.

Mtaji wa kianzio cha Ufugaji wa ng'ombe

Vijana wengi wa kitanzania hulalamika kutokuwa na mtaji ya kutosha kwa ajili ya shughuli za ufugaji ng'ombe, pasipo kujua kwamba kiasi kidogo walichonacho wanaweza kuanza nacho hata ikiwa ni mtaji wa ng'ombe mmoja.

Kwa upande wa vijana wa Simiyu, wengi walianza na ng'ombe mmoja hadi wawili na watatu, na ukiangalia kwa sasa wengine hadi sasa wamefikisha idadi ya ng'ombe wengi ambapo Dk. Nawanda alianza na mtaji wa ng'ombe 10, mwaka 2022 alipofika Simiyu na kufika mwaka 2023 alikuwa na ng'ombe zaidi ya 70.

Mara baada ya kuuza ng'ombe hao alipata kiasi cha fedha sh. milioni 31 ambayo kwa mujibu wake anakiri hakuna biashara aliyowahi kufanya ikamlipa kiasi hicho.

Kufuatia faida hiyo aliamua kujikita katika shughuli hiyo ya unenepeshaji ambapo sasa kazi yake imekuwa ni kununua chakula cha ng'ombe, kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na mahitaji mbalimbali ya muhimu kwa ajili ya shughuli hiyo.

Kwa sasa hivi ng'ombe mmoja mkoani Simiyu baada ya kumnenepesha, unaweza kumuuza hadi sh. milioni 1.4 ambayo kwa idadi ya ng'ombe 70 alionao anaweza kupata hadi milioni 91 ambayo kimsingi inatokana na kazi aliyoifanya kwa miezi mitatu tu.

Chakula cha ng'ombe kwa ajili ya unenepeshaji

Mahitaji makuu ya shughuli ya unenepeshaji mbali na eneo ni pamoja na pumba ya mpunga au mahindi, mashudu ya pamba na chumvi ambavyo vyote vinapatikana mkoani Simiyu, ambapo mashudu na pumba yanapatikana Lamadi na chumvi ya mawe inapatikana Meatu.

Soko la Ng'ombe anaowanenepesha

Mkoani Simiyu kuna mnada maarufu sana unaojulikana kama mnada wa Kidinda na hapo ndipo ambapo Dk. Nawanda hununua ng'ombe anaotaka kuwanenepesha na wakishanenepa hutumia mnada huo huo kuwauza kwa wafanyabiashara wa ndani na nje ya mkoa huo na nchi kwa ujumla.

Maelekezo kwa Maofisa Mifugo mkoani Simiyu.

Kufuatia kile anachokifanya kuzaa matunda na kuonesha kuwanufaisha wengi, Dk. Nawanda aliwaagiza maofisa mifugo waliopo mkoani humo kuhakikisha wanafanya shughuli za ufugaji wawe mfano bora kwa wakazi waliopo maeneo yao na kuhamasisha ufugaji bora kwa ujumla.

Hakika Dk. Nawanda ameonesha dira si tu kwa wakazi wa mkoa wa Simiyu bali kwa Watanzania wote walioukuwa na shauku ya kufanya shughuli ya unenepeshaji wa Mifugo.

CamScanner